AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi : +251 115 517 844
Tuvuti : www.au.int

BARAZA KUU
Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Nne
Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1483(XLIV)Rev.1
Matini chanzi: Kiingereza

RIPOTI KUHUSU KATIBA YA JOPO LA WAAFRIKA MAARUFU WATAKAOSIMAMIA UCHAGUZI WA AWALI WA WAJUMBE WA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA

RIPOTI KUHUSU KATIBA YA JOPO LA WAAFRIKA MAARUFU WATAKAOSIMAMIA UCHAGUZI WA AWALI WA WAJUMBE WA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA

1. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa sasa wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika walichaguliwa mwaka 2021 kwa muhula wa miaka minne ambao unaisha Februari 2025. Kuhusiana na hili, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu watachagua Kamisheni mpya mwezi Februari 2025.

2. Mchakato wa uteuzi wa awali wa Wajumbe wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika umekabidhiwa kwa Jopo la Waafrika Mashuhuri ("Jopo") kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 13 na 15 ya Sheria ya Mkataba wa Kamisheni (Sheria ya Mkataba) kama ifuatavyo:

Kifungu cha 13
Uteuzi wa Makamishna

Tathmini ya ustadi na umahiri na uteuzi wa wagombea utafanywa na Jopo la Ngazi ya Juu la Waafrika Mashuhuri (1 kwa kila kanda) wakisaidiwa na kampuni huru ya Kiafrika ili kutoa kundi la wagombea wateule wa awali na kanda husika za AU ambako Makamishna watachaguliwa na kuteuliwa na Baraza Kuu.

Kifungu cha 15
Jopo la Waafrika Mashuhuri

1. *Jopo la Waafrika Mashuhuri litaundwa na watu mashuhuri watano (5), mmoja (1) kwa kila kanda.*

2. *Jopo la Waafrika Mashuhuri litasimamia uteuzi wa awali wa wagombea wa nafasi ya Mjumbe wa Kamisheni na litapewa ushauri wa kitaalam na kampuni huru ya ushauri ya Kiafrika, itakayochaguliwa na Jopo.*

3. *Wasifu wa kazi na vigezo vya umahiri kwa nafasi ya juu ya Uongozi wa Kamisheni vitaandaliwa na Jopo la Waafrika Mashuhuri. Hivi vitajumuisha ujuzi na uwezo wa jumla wa uongozi pamoja na ujuzi wa kitaalamu na mada kuhusiana na nafasi maalum. Pamoja na kanuni muhimu zilizorejelewa hapo juu, mchakato wa tathmini kwa wagombea wote utazingatia ujuzi na uwezo ulioainishwa kwa kila nafasi ya juu ya uongozi.*

3. Ili kuratibu katiba ya Jopo, Kamisheni kupitia Dokezo lake lenye Namba ya kumbukumbu BC/OLC/217/13875.23 ya tarehe 16 Oktoba 2023 iliwaalika Wakuu wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kuratibu mashauriano ya kikanda kwenye maeneo yao na kuteua Mjumbe mmoja(1) kwa kila Kanda ifikapo tarehe 30 Novemba 2023.

4. Kufikia tarehe 30 Novemba 2023, ni Kanda ya Kusini pekee ndiyo iliyowasilisha mteule wake. Kwa maana hiyo, uwasilishaji wa wateule, mmoja kila moja ya kanda zifuatazo: Kanda ya Kati, Mashariki, Kaskazini na Magharibi ulisogezwa hadi tarehe 15 DESEMBA 2023.

5. Katika Dokezo hilohilo, Kamisheni ilitoa wito kwa Mkuu wa Kanda ya Kiuchumi ya Kaskazini, ambaye alikuwa amewasilisha wagombea kadhaa, kuratibu mashauriano ya kumpata mgombea mmoja ili kuiwakilisha kanda hiyo.

6. Kufikia tarehe 15 Desemba 2023, Kamisheni ilikwishapokea mapendekezo kutoka Kanda za Kusini, Magharibi na Mashariki. Ingawa Kanda ya Kaskazini ilikwishawasilisha wagombea kadhaa, hakukuwa na uteuzi kutoka Kanda ya Kati. Kwa hivyo Kamisheni, kupitia Dokezo lenye namba ya kumbukumbuBC/OLC/217/14225.23 la tarehe 19 Desemba, 2023 iliongeza muda wa mwisho wa kuwasilisha uteuzi kutoka Kanda ya Kati hadi tarehe 30 Desemba 2023.

7. Tarehe 21 Desemba 2023, Kamisheni ilipendekeza kuratibu uteuzi wa mgombea mmoja kutoka kanda ya Kaskazini, mpango ambao haukukubaliwa na Kanda hiyo.

8. Kufikia tarehe 30 Desemba 2023, yafuatayo yalikuwa majina ya wateule kutoka kanda husika:

	JINA	**JINSIA**	**NCHI**	**KANDA**
1	Konjit SineGiorgis	KE	Ethiopia	Mashariki
2	Nozipho Joyce Mxakato-Diseko	KE	Afrika Kusini	Kusini
3	Patrick Hayford	ME	Ghana	Magharibi
4	Djinnit Said	ME	Algeria	Kaskazini
5	Mohamed Adel Smaoui	ME	Tunisia	Kaskazini
6	Lehcen Haddad	ME	Morocco	Kaskazini
7	Sidi Salem Mohamed Alabd	ME	Mauritania	Kaskazini
8	Achraf Rached	ME	Misri	Kaskazini
9	Ali Abdallah Awidan	ME	Libya	Kaskazini

9. Kanda za Kaskazini na Kati zitalazimika kuendelea na mashauriano ya kikanda ili kuwasilisha mapendekezo yao. Hata hivyo, ili kukidhi muda ulioainishwa kwenye sheria ya Mkataba, ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwa wagombea kwa wajumbe wa Kamisheni mwezi Machi, 2024 kwa mujibu wa Kifungu cha 16(a) cha Sheria ya Mkataba, Jopo lazima liundwe na kuteuliwa wakati wa Kikao cha sasa. Jambo hili litawawezesha kuanza kutekeleza majukumu yao mara moja, ikiwa ni pamoja na kuteua kampuni ya ushauri itakayowasaidia katika majukumu yao.

10. Hivyo inapendekezwa kuwa Wajumbe watatu (3) wa kuteuliwa kutoka Kanda ya Mashariki, Kusini na Magharibi wapitishwe na wapewe mamlaka ya kuanza kutekeleza majukumu yao huku wakisubiri katiba ya jopo kamili.

11. Inapendekezwa zaidi kwamba Baraza Kuu limpe Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ridhaa ya kupitisha Wajumbe wawili (2) waliobaki kutoka Kanda ya Kati na Kaskazini mtawalia, **mara baada ya mashauriano ya kikanda kukamilika.**

RASIMU YA UAMUZI KUHUSU KATIBA YA JOPO LA WAAFRIKA MAARUFU

Baraza Kuu,

1. **LINAPOKEA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Katiba ya Jopo la Waafrika Mashuhuri kwaajili ya kusimamia uteuzi wa awali wa Wajumbe wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

2. **LINAWATHIBITISHA** wafuatao kama Wajumbe wa Jopo la Watu Mashuhuri wa Afrika ili kusimamia uteuzi wa awali wa Wajumbe wa Kamisheni kwa ajili ya uchaguzi uliopangwa kufanyika mwaka 2025.

NO.	JINA	JINSIA	NCHI	KANDA
1.				
2.				
3.				

3. **LINATOA MAMLAKA** kwa Wajumbe wa jopo watatu (3) walioidhinishwa Kuanza kutekeleza majukumu yao kwa hatua ya haraka, kwa kusubiria uundaji wa jopo kamili.

4. **LINATOA WITO** kwa Kanda za Kati na Kaskazini kuharakisha hitimisho la mashauriano ya kikanda na kuwasilishwa kwa mteuliwa mmoja(1) kwa kila ukanda, kumalizia uundaji wa jopo.

5. **LINAAMUA** kumpa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika idhini ya kupitisha Wajumbe wawili (2) waliobaki wa Jopo kutoka Kanda za Kati na Kaskazini baada ya kanda za Kati na Kaskazini kuwasilisha mteuliwa mmoja.

6. **LINAAMUA ZAIDI** kwa mujibu wa Kanuni ya 35 ya Kanuni za Taratibu za Mkutano Mkuu, kwa uamuzi huu kuchukua hatua ya haraka baada ya kupitishwa kwake ili kuendana na ratiba ya uchaguzi iliyooneshwa kwenye Sheria ya Mkataba ya Kamisheni.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-02-15

Report on the Constitution of the Panel of Eminent Africans to oversee the pre-Selection of Members of the African Union Commission

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10521

Downloaded from African Union Common Repository